ISSN 0856-6976

# MUHTASARI WA TAMKO LA SERA YA FEDHA

*Mapitio ya Nusu Mwaka*
**2018/19**

**GAVANA**
**BENKI KUU YA TANZANIA**

**Februari 2019**

ISSN 0856-6976

# MUHTASARI WA TAMKO LA SERA YA FEDHA

## *Mapitio ya Nusu Mwaka*

## 2018/19

**GAVANA**

**BENKI KUU YA TANZANIA**

**Februari 2019**

## Utangulizi

Taarifa hii ya mapitio ya Tamko la Sera ya Fedha inatathmini mwenendo wa utekelezaji wa Sera ya Fedha katika kipindi cha nusu ya kwanza ya mwaka wa fedha 2018/19, na mwenendo wa sasa na wa baadaye wa hali ya uchumi, na kuainisha mwelekeo wa kisera ambao Benki Kuu inakusudia kuchukua katika kipindi kilichobakia cha mwaka 2018/19.

## Mwenendo wa Uchumi wa Dunia

Kulingana na taarifa ya mwelekeo wa hali ya uchumi wa dunia iliyotolewa na Shirika la Fedha la Kimataifa (International Monetary Fund (IMF)) mwezi Januari 2019, uchumi wa dunia unakadiriwa kukua kwa wastani wa asilimia 3.7 mwaka 2018, ikilinganishwa na wastani wa asilimia 3.8 mwaka 2017. Ukuaji wa uchumi wa dunia ulichangiwa zaidi na kuimarika kwa uchumi wa Marekani, wakati ukuaji kwa nchi za Ulaya na Asia ukipungua. Ukuaji wa Pato la Taifa nchini Marekani umebakia kuwa imara, ukikua kwa asilimia 2.9 mwaka 2018, ikilinganishwa na asilimia 2.2 mwaka 2017, kulikochangiwa zaidi na sera ya kibajeti. Aidha, ukuaji katika nchi za Ulaya ulipungua hadi asilimia 1.8 mwaka 2018 kutoka asilimia 2.4 mwaka 2017, kutokana na kupungua kasi ya mauzo ya nje kufuatia kuimarika kwa sarafu ya euro na kupungua kwa mahitaji ya nje. Ukuaji wa uchumi nchini Uingereza ulipungua na kufikia asilimia 1.4 kutoka asilimia 1.8, hasa kwa sababu ya matumizi dhaifu ya ndani yanayohusiana na hofu ya kujitoa kutoka jumuiya ya Ulaya (Brexit). Ukuaji wa uchumi nchini Japan ulipungua hadi asilimia 0.9 kutoka asilimia 1.9, kutokana na kudorora kwa shughuli za kiuchumi katika robo ya kwanza na ya tatu, kulikosababishwa na hali mbaya ya hewa na maafa.

Ukuaji wa uchumi wa nchi zinazoibukia kiuchumi na zile zinazoendelea kukua ulifikia asilimia 4.6 mwaka 2018 kutoka asilimia 4.7 mwaka 2017, hali iliyochangiwa zaidi na kuimarika kwa dola ya Marekani, kupungua kwa mitaji, kuongezeka kwa mvutano wa kibiashara na kupungua kwa uzalishaji viwandani na biashara ya kimataifa. Ukuaji wa uchumi nchini China ulipungua hadi asilimia 6.6 mwaka 2018 kutoka asilimia 6.9 mwaka 2017, ukichangiwa zaidi na kuongezeka kwa mahitaji ya ndani pamoja na uwekezaji, hali iliyosaidia kupunguza athari ya kupungua kwa mauzo ya nje. Ukuaji wa uchumi wa nchi za kusini mwa jangwa la Sahara umeendelea kuimarika katika mwaka 2018, japo kwa kasi ya chini. Ukuaji katika eneo hilo unakadiriwa kubakia katika asilimia 2.9 kwa mwaka 2018, sawa na kiwango kilichofikiwa mwaka 2017. Hali hii imechangiwa zaidi na kudorora kwa ukuaji wa uchumi wa Angola, Nigeria na Afrika Kusini.

Kulingana na taarifa ya mwelekeo wa hali ya uchumi wa dunia iliyotolewa na Shirika la Fedha la Kimataifa (IMF) mwezi Januari 2019, ukuaji wa uchumi wa dunia unakadiriwa kuwa asilimia 3.5 kwa mwaka 2019 na asilimia 3.6 mwaka 2020. Ukuaji wa uchumi wa mataifa yaliyoendelea unakadiriwa kupungua na kufikia asilimia 2.0 mwaka 2019 na asilimia 1.7 mwaka 2020. Ukuaji wa uchumi katika nchi zinazoibukia kiuchumi na zile zinazoendelea kukua, unatarajiwa kupungua hadi kufikia asilimia 4.5 mwaka 2019, kabla ya kuongezeka na kufikia asilimia 4.9 mwaka 2020. Katika nchi za kusini mwa jangwa la Sahara, ukuaji wa uchumi unakadiriwa kuongezeka na kufikia asilimia 3.5 mwaka 2019 na asilimia 3.6 mwaka 2020, hii inatokana na kupungua kwa sera za kiuchumi zisizotabirika, kuongezeka kwa uwekezaji wa mataifa makubwa, pamoja na ukuaji wa kasi wa nchi zisizo na rasilimali.

Viwango vya mfumuko wa bei katika nchi zilizoendelea na zile zinazoibukia kiuchumi vimeendelea kubaki katika viwango vya chini kutokana na kushuka kwa bei ya chakula, nguo na viatu. Katika nchi za Jumuiya ya Afrika ya Mashariki (EAC) na Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC), wastani wa mfumuko wa bei ulipungua ukichangiwa zaidi na kushuka kwa bei za chakula. Kulingana na taarifa ya mwelekeo wa hali ya uchumi wa dunia iliyotolewa na Shirika la Fedha la Kimataifa (IMF) mwezi Januari 2019, kiwango cha mfumuko wa bei katika nchi zilizoendelea unatarajiwa kufikia wastani wa asilimia 1.7 mwaka 2019, kutoka asilimia 2.0 mwaka 2018. Wakati huohuo, mfumuko wa bei katika nchi zinazoibukia kiuchumi na zile zinazoendelea kukua unatarajiwa kuongezeka hadi kufikia wastani wa asilimia 5.1 mwaka 2019, kutokana na kupanda kwa bei za vyakula.

## Mwenendo wa Uchumi wa Tanzania

### Tanzania Bara

Uchumi wa Tanzania umeendelea kuimarika, ambapo katika kipindi cha robo tatu za mwanzo wa mwaka 2018, uchumi ulikua kwa wastani wa asilimia 6.7 ikilinganishwa na ukuaji wa wastani wa asilimia 6.2 kwa kipindi kama hicho kwa mwaka 2017[1]. Shughuli za kiuchumi zilizokua kwa kasi zaidi ni pamoja na ujenzi, biashara, kilimo na viwanda.

Katika kipindi cha nusu ya kwanza ya mwaka wa fedha 2018/19, mfumuko wa bei uliendelea kushuka na kubakia chini ya lengo la muda wa kati la asilimia 5.0 na ndani ya vigezo vya muunganiko wa kiuchumi katika

[1] Kizio cha mwaka 2007

Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC) na Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC). Hali hii ilichangiwa na kuongezeka kwa uzalishaji wa chakula, utulivu katika thamani ya shilingi ya Tanzania dhidi ya dola ya Marekani na sarafu nyingine kubwa duniani na utekelezaji thabiti wa sera ya fedha na ya kibajeti. Katika kipindi cha nusu ya kwanza ya mwaka wa fedha 2018/19, mfumuko wa bei ulikuwa wastani wa asilimia 3.2 ikilinganishwa na asilimia 4.8 katika kipindi kama hicho mwaka 2017/18. Katika kipindi hicho, mfumuko wa bei usiojumuisha bei za vyakula na nishati (*core inflation*) ulikuwa wastani wa asilimia 2.3 ukilinganishwa na asilimia 1.7.

Katika kipindi cha nusu ya kwanza ya mwaka wa fedha 2018/19, mapato yaliyokusanywa na kuwekwa kwenye akaunti za Serikali zilizoko Benki Kuu ya Tanzania yalikuwa shilingi bilioni 8,740.8, kiasi ambacho kilikuwa ni asilimia 3.6 zaidi ya mapato yaliyokusanywa na kuwekwa kwenye akaunti hizo katika kipindi kama hicho mwaka 2017/18. Aidha, kiasi hicho ni sawa na asilimia 95.3 ya makadirio ya makusanyo katika kipindi cha miezi sita ya kwanza ya mwaka 2018/19. Kuongezeka kwa makusanyo ya mapato kwa sehemu kubwa kumetokana na jitihada zinazotekelezwa na Serikali katika kuongeza matumizi ya teknolojia katika ukusanyaji wa kodi kupitia Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA), na kuongezeka kwa ukusanyaji wa mapato yasiyo ya kodi. Katika kipindi hicho, jumla ya matumizi ya Serikali yaliyofanywa kupitia katika akaunti zake zilizoko Benki Kuu yalifikia shilingi bilioni 9,207.2. Shilingi bilioni 6,880.3 zilikuwa ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida, na shughuli za maendeleo ziligharimu shilingi bilioni 2,326.9.

Katika kipindi cha nusu ya kwanza ya mwaka wa fedha 2018/19, urari wa malipo nje ya nchi (*balance of payments*) ulikuwa na nakisi ya dola za Marekani milioni 471.0 ikilinganishwa na ziada ya dola za Marekani milioni 963.9 katika kipindi kama hicho mwaka 2017/18. Hali hii ilisababishwa na kuongezeka kwa nakisi ya urari wa biashara ya bidhaa, huduma na uhamisho mali nchi za nje (*current account*). Nakisi ya urari wa biashara ya bidhaa, huduma na uhamisho mali nchi za nje iliongezeka na kufikia dola za Marekani milioni 1,297.1 ikilinganishwa na nakisi ya dola za Marekani milioni 658.9 katika kipindi kama hicho mwaka 2017/18. Hali hii ilichangiwa na kuongezeka kwa thamani ya bidhaa za mitaji zilizoagizwa kutoka nje ya nchi kwa ajili ya miradi mikubwa ya maendeleo, hasa ya miundombinu.

Akiba ya fedha za kigeni imeendelea kuwa ya kuridhisha na kuendelea kukidhi mahitaji ya fedha za kigeni kwa ajili ya kuagiza bidhaa na huduma nje ya nchi. Akiba ya fedha za kigeni ilifikia dola za Marekani milioni 5,044.6 mwishoni mwa mwezi Desemba 2018, ambayo inatosha kulipia uagizaji wa bidhaa na huduma kutoka nje ya nchi kwa kipindi cha takriban miezi 4.9, kiasi ambacho ni juu ya lengo la nchi la kukidhi miezi isiyopungua 4.0. Rasilimali za fedha za kigeni za benki za biashara zilikuwa dola za Marekani milioni 966.7 hadi kufikia mwisho wa mwezi Desemba 2018.

Tathmini ya Benki ya Dunia juu ya usimamizi wa sera za nchi na taasisi zake (*Country Policy and Institutional Assessment* (CPIA)) uliofanyika mwaka 2018, uliiweka nchi ya Tanzania katika kundi la nchi zenye sera imara, taasisi na ukuaji wa uchumi thabiti. Kufuatia hatua hii, vizingiti vya

uhimilivu wa deni la Taifa viliongezeka na kutoa wigo mpana zaidi wa nchi kuweza kukopa kutoka katika vyanzo vya nje ya nchi. Matokeo ya awali ya uchambuzi wa uhimilivu wa deni la Taifa (Debt Sustainability Analysis (DSA)), uliofanyika mwezi Desemba mwaka 2018 kwa kutumia kiwango cha deni la Taifa mwishoni mwa mwezi Juni 2018 na viashiria vipya vya CPIA, inaonyesha kwamba deni la nje la Taifa ni himilivu kulingana na viashiria vyote vya uendelevu. Hadi kufikia mwezi Desemba 2018, deni la sekta ya umma lilipungua na kufikia kiasi cha dola za Marekani milioni 22,530.5, kutoka dola za Marekani milioni 22,760.4 mwezi Juni 2018. Kupungua huku kulitokana na kuiva kwa dhamana na hati fungani za Serikali. Hadi kufikia mwishoni mwa mwezi Desemba 2018, madeni ya nje ya sekta ya umma yalichangia asilimia 71.7 ya jumla ya madeni yote ya umma.

Katika kipindi cha nusu ya kwanza ya mwaka 2018/19, sekta ya kibenki imeendelea kuwa imara, salama na yenye kutengeneza faida, ikiwa na mitaji na ukwasi wa kutosha zaidi ya kiwango kinachotakiwa kisheria. Benki Kuu imeendelea kuchukua hatua mbalimbali za kuimarisha sekta ya kibenki hasa katika kupunguza uwiano wa mikopo chechefu kufikia lengo la chini ya asilimia 5.0. Baadhi ya hatua zilizochukuliwa ni pamoja na kuzitaka benki na taasisi za fedha: kuboresha usimamizi katika utoaji mikopo; kuwasilisha mpango kazi ya jinsi ya kupunguza uwiano wa mikopo chechefu kwa benki zilizokuwa na uwiano mkubwa; na kutumia kwa lazima taarifa ya historia za wakopaji (*credit reference bureau reports*) kabla ya utoaji wa mikopo. Hatua hizi ziliweza kuchangia kupungua kwa uwiano wa mikopo chechefu hadi kufikia asilimia 10.4 ya mikopo yote mwezi Desemba 2018 kutoka asimilia 11.3 kwa mwezi Juni 2018.

Wakati huo huo, Benki Kuu imeendelea kusimamia utekelezaji wa hatua za kuimarisha udhibiti wa vihatarishi katika sekta ya fedha (*risk management practices*) kwa kupitia upya kanuni na miongozo[2] mbalimbali ili iendane na mabadiliko ya sasa. Hii inajumuisha miongozo kwa ajili ya wakurugenzi wa benki na taasisi za fedha ikiwa ni moja ya jitihada za kuboresha usimamizi wa sekta ya fedha nchini. Pia Benki Kuu imeendelea kuboresha mfumo wa wakala wa benki na taratibu za ukaguzi wa mfumo huo. Benki Kuu imeendelea pia katika kupitia vigezo vipya vya Basel II/III na kuchambua na kufafanua mahitaji ya vigezo hivyo kwenye mitaji ya benki na utoshelevu wa ukwasi. Benki Kuu ilishiriki katika mapitio ya uboreshaji wa Sera ya Taasisi ndogo za Fedha (*National Microfinance Policy*) pamoja na kuandaa rasimu ya Muswada wa Sheria ya Taasisi ndogo za Fedha (*National Microfinance Bill*), ambapo sheria hii ilipitishwa na Bunge mwezi Novemba 2018. Sheria hii inalenga kuongeza usimamizi kwa taasisi ndogo za fedha na zile zinazotoa mikopo pekee ili kumlinda mteja ambapo Benki Kuu imepewa jukumu la kusimamia taasisi hizo.

Katika kipindi cha nusu ya kwanza ya mwaka 2018/19, mifumo ya malipo iliendelea kufanya kazi kwa ufanisi. Kuanzia Julai 2018, malipo yote ya serikali yalianza kufanyika kupitia mfumo wa Akaunti Moja ya Hazina (*Treasury Single Account*, (TSA)) kupitia mfumo wa kielektroniki wa kuhamisha fedha kutoka katika akaunti ya benki moja hadi nyingine (*Tanzania Automated Clearing House,* (TACH)) na mfumo wa malipo wa Benki Kuu ya Tanzania (*Tanzania Interbank Settlement System,* (TISS)) (kwa miamala ya zaidi ya shilingi milioni 10). Matumizi ya mifumo hii ya malipo imewezesha serikali kuongeza ufanisi katika malipo hasa ya mishahara na kupunguza gharama zinazoambatana na malipo kupitia hundi.

2 Guidelines for Directors of Banks and Financial Institutions; the Outsourcing Guidelines; Business Continuity Management Guidelines

Aidha, mfumo wa malipo wa Afrika ya Mashariki (*East Africa Payment System,* (EAPS)) uliendelea kufanya kazi kwa ufanisi ikiwa ni pamoja na kuongezeka kwa miamala ndani ya mfumo huo hali inayoashiria ongezeko la shughuli za kiuchumi baina ya Tanzania na nchi nyingine za Jumuiya ya Afrika Mashariki.

Katika kipindi cha nusu ya kwanza ya mwaka 2018/19, utoaji wa huduma za kifedha baina ya mitandao ya simu kupitia simu za mikononi uliendelea kuongezeka kwa kasi ya kuridhisha. Katika kipindi hicho, miamala inayotumia simu za mikononi ilikuwa milioni 83.4 ikiwa yenye thamani sawa na shilingi bilioni 2,897.8, ikiwa ni ongezeko la asilimia 85.7 na asilimia 52.1 ikilinganishwa na miamala iliyofanyika na thamani iliyopatikana katika kipindi kama hicho mwaka 2017/18, kwa mtiririko huo. Hadi kufikia mwezi Desemba 2018, Watanzania wapatao milioni 23.3 walikuwa watumiaji hai wa miamala kwenye mfumo wa malipo kupitia simu za mikononi, ikilinganishwa na Watanzania milioni 19.4 waliokuwepo mwishoni mwa mwezi Desemba 2017.

**Zanzibar**

Katika kipindi cha nusu ya kwanza ya mwaka 2018, ukuaji halisi wa Pato la Taifa la Zanzibar lilifikia wastani wa asilimia 5.5 ikilinganishwa na asilimia 7.5 katika kipindi kama hicho mwaka 2017. Ukuaji huo ulitokana na kuongezeka kwa shughuli za utalii hususan malazi na huduma ya chakula; ujenzi miundombinu na majengo; kilimo; na shughuli za viwandani. Ukuaji wa uchumi unatarajiwa kuendelea kuimarika katika kipindi cha nusu ya pili ya mwaka 2018, ukichangiwa zaidi na utekelezaji endelevu

wa miradi ya maendeleo, kuongezeka kwa huduma za kitaalamu kwenye kilimo, kuimarika kwa kilimo cha maua na mboga pamoja na utalii.

Katika kipindi cha nusu ya kwanza ya mwaka 2018/19, mfumuko wa bei ulifikia wastani wa asilimia 3.8, kiwango ambacho ni chini ya lengo la muda wa kati la asilimia 5.0. Hali hii ilichangiwa zaidi na kushuka kwa bei za vyakula hususan ndizi na sukari. Aidha, mfumuko wa bei unategemewa kuendelea kuwa chini ya tarakimu moja katika kipindi cha nusu ya pili ya mwaka 2018/19, licha ya kuwa na uwezekano wa bei za bidhaa kupanda katika soko la dunia, hususan bei ya mafuta.

Katika kipindi cha nusu ya kwanza ya mwaka 2018/19, mapato ya ndani ya Serikali yalifikia shilingi bilioni 395.5, sawa na asilimia 92.0 ya makadirio ya makusanyo kwa kipindi hicho. Mapato yatokanayo na kodi yalikuwa shilingi bilioni 322.8, wakati mapato yasiyotokana na kodi yalikuwa shilingi bilioni 36.7. Jumla ya matumizi ilikuwa shilingi bilioni 505.6; kati ya hizo, matumizi ya kawaida yalikuwa shilingi bilioni 360.1 na matumizi ya maendeleo shilingi bilioni 145.5.

Urari wa biashara ya bidhaa, huduma na uhamisho mali nchi za nje ulikuwa na nakisi ya dola za Marekani milioni 35.8 katika kipindi cha nusu ya kwanza ya mwaka 2018/19, ikilinganishwa na ziada ya dola za Marekani milioni 34.4 katika kipindi kama hicho mwaka 2017/18. Hali hii ilichangiwa zaidi na kuongezeka kwa uagizaji wa bidhaa nchi za nje, hususan mafuta na chakula pamoja na kupungua kwa mauzo ya karafuu nje ya nchi.

## Utekelezaji wa Malengo ya Sera ya Fedha ya Mwaka 2018/19

### *Malengo ya Sera ya Fedha*

Katika kipindi cha nusu ya kwanza ya mwaka 2018/19, Benki Kuu ya Tanzania iliendelea kutekeleza sera ya fedha iliyolenga kudumisha kiwango cha kutosha cha ukwasi kwenye uchumi unaoendana na mahitaji ya malengo mapana ya kiuchumi ya serikali ya kusimamia utulivu wa bei na kiwango cha juu cha ukuaji uchumi. Ili kufikia malengo ya Serikali ya uchumi mpana kwa mwaka 2018/19, Benki Kuu inaendelea kutekeleza sera ya fedha inayolenga kuwepo kwa utulivu wa bei na riba katika masoko ya fedha. Katika mwaka 2018/19, Benki Kuu imeweka malengo yafuatayo:

i. Ukuaji wa wastani wa fedha taslim usiozidi asilimia 11.5;

ii. Ukuaji wa ujazi wa fedha kwa tafsiri pana zaidi (M3) usiozidi asilimia 12.2;

iii. Ukuaji wa mikopo kwa sekta binafsi usiozidi asilimia 10.2; na

iv. Kuwa na akiba ya fedha za kigeni inayotosha kuagiza bidhaa na huduma kutoka nje ya nchi kwa kipindi kisichopungua miezi minne.

### *Utekelezaji wa Sera ya Fedha kwa Kipindi cha Nusu ya Kwanza ya Mwaka 2018/19*

Katika kipindi cha nusu ya kwanza ya mwaka 2018/19, Benki Kuu ilichukua hatua mbalimbali za kuongeza ukwasi kwenye uchumi ili kuziwezesha benki na taasisi za fedha kuongeza ukuaji wa mikopo kwa sekta binafsi na kwa uchumi mzima kwa ajili ya kuendeleza shughuli mbalimbali za uchumi. Njia zilizotumika katika kuongeza ukwasi kwenye uchumi ili kuendana na mahitaji ni pamoja na kununua fedha za kigeni kutoka katika

benki za biashara na taasisi za serikali, kutoa mikopo ya muda mfupi kwa mabenki, na kushusha riba ya mikopo kwa mabenki (*discount rate*) kulikofanywa mwezi Agosti 2018 kutoka asilimia 9.0 hadi asilimia 7.0.

Katika kipindi cha nusu ya kwanza ya mwaka 2018/19, riba ya siku moja katika soko la fedha baina ya mabenki (*overnight interbank cash market rate*) imeendelea kuwa tulivu ambapo imeendelea kubakia kati ya wastani wa asilimia 1.89 na asilimia 2.98. Hata hivyo, kulitokea ongezeko kubwa la mahitaji ya shilingi kwa ajili ya malipo ya kodi za makampuni na sherehe za mwisho wa mwaka 2018. Aidha, riba za dhamana za serikali ziliongezeka sambamba na hali ya ukwasi katika uchumi. Wastani wa riba za mikopo inayotolewa na mabenki imeendelea kuwa juu pamoja na hatua za kuongeza ukwasi zilizochukuliwa na Benki Kuu. Benki Kuu, kwa kushirikiana na wadau mbalimbali, inaendelea kuchukua hatua mbalimbali za kuhakikisha kuwa riba za mikopo zinakuwa na unafuu na kuendana na hali halisi ya uchumi. Hatua hizo ni pamoja na mabenki kupata taarifa sahihi za wakopaji kwa kutumia kanzidata ili kupunguza mikopo chechefu, pamoja na marekebisho ya sheria katika usimamizi wa masuala ya fedha nchini.

Ujazi wa fedha kwa tafsiri pana zaidi (*extended broad money supply, M3*) umekua kwa wastani, wakati ukuaji wa mikopo kwa sekta binafsi ikiendelea kuimarika. Ukuaji wa mwaka wa ujazi wa fedha kwa tafsiri pana zaidi ulifikia asilimia 4.5 mwezi Desemba 2018 kutoka asilimia 6.0 mwezi Juni 2018. Aidha, ukuaji huu wa fedha unaakisi ongezeko la matumizi ya kielektroniki katika kufanya malipo, hali ambayo imejitokeza katika kuongezeka kwa kasi ya mzunguko wa fedha. Mikopo kwa sekta

binafsi imeendelea kukua na kufikia asilimia 4.9 mwezi Desemba 2018, ikilinganishwa na ukuaji wa wastani wa asilimia 4.0 na asilimia 1.7 katika miezi ya Juni 2018 na Desemba 2017, kwa mtiririko huo. Ukuaji wa mikopo kwa sekta binafsi unatarajiwa kuendelea kuimarika sambamba na muendelezo wa utekelezaji wa sera ya fedha inayolenga kuendelea kuongeza ukwasi, pamoja na hatua zinazochukuliwa katika kupunguza mikopo chechefu na kuboresha mazingira ya kufanya biashara nchini.

Thamani ya shilingi ya Tanzania dhidi ya dola ya Marekani imeendelea kuwa tulivu kwa kipindi chote cha nusu ya kwanza ya mwaka 2018/19. Hali hii ilitokana na utekelezaji mzuri wa sera ya fedha, usimamizi thabiti wa mapato na matumizi ya serikali, matumizi ya gesi asilia badala ya mafuta katika kuzalisha umeme, na baadhi ya viwanda kuzalisha bidhaa ambazo awali zilikuwa zikiagizwa kwa wingi kutoka nje kama vile vigae.

Katika kipindi cha nusu ya kwanza ya mwaka 2018/19, Benki Kuu imeendelea na hatua za matayarisho ya mfumo mpya wa utekelezaji wa sera ya fedha unaotumia riba ya Benki Kuu (*central bank policy rate*) ikiwa ni pamoja na: kukamilisha kanuni za ushiriki katika mfumo wa soko la fedha baina ya mabenki (*inter-bank cash market system code of conduct*) na uboreshaji wa mfumo wa dhamana (*collateral framework*). Maeneo mengine yaliyoboreshwa ni pamoja na kuunganisha mfumo wa soko la dhamana za serikali na hati fungani (*BOT's Central Securities Depositories,* (*CSD*)) na ule wa dhamana wa soko la mitaji (*Dar es Salaam Stock Exchange* (*CDS*)). Pia, mfumo wa kielektoniki wa soko la fedha baina ya mabenki ulianza kufanya kazi rasmi mwezi Novemba 2018 hatua ambayo itaboresha upatikanaji wa viashiria halisi vya ukwasi nchini na kusaidia usimamizi wa utekelezaji wa sera ya fedha.

*Matarajio ya Uchumi*

Pato la Taifa linakadiriwa kukua kwa asilimia 7.2 mwaka 2018 na 7.3 mwaka 2019, ikichangiwa kwa kiasi kikubwa na: uwekezaji wa umma kwenye miundombinu ya barabara, reli, umeme, bandari, na viwanja vya ndege; matarajio ya hali nzuri ya hewa itakayoongeza uzalishaji wa chakula; na matarajio ya kuimarika kwa uchumi wa dunia[3]. Pia mageuzi ya kiuchumi kupitia hatua mbalimbali ambazo serikali inaendelea kuzichukua katika kuongeza ubora na thamani katika mazao na bidhaa za madini na kilimo ikiwamo sera ya viwanda, vinatarajiwa kuongeza msukumo katika ukuaji wa uchumi. Kuongezeka kwa mikopo kwa sekta binafsi na hatua zinazochukuliwa katika kupunguza mikopo chechefu na kuboresha mazingira ya kufanya biashara vinatarajiwa kuongeza kasi ya ukuaji wa uchumi.

Mfumuko wa bei unatarajiwa kuendelea kubakia ndani ya lengo la asilimia 5 katika nusu ya pili ya mwaka wa fedha 2018/19. Hali hii itachangiwa zaidi na kuimarika kwa uzalishaji wa chakula, uzalishaji wa umeme na muendelezo wa sera thabiti ya fedha na kibajeti; pamoja na kuendelea kuwepo kwa utulivu wa thamani ya shilingi dhidi ya dola ya Marekani na sarafu nyingine duniani. Hata hivyo, makubaliano ya kupunguza uzalishaji wa mafuta yaliyofikiwa baina ya nchi zinazozalisha mafuta kwa wingi duniani (OPEC) yanaweza yakaathiri kasi ya mfumuko wa bei.

Nakisi ya urari wa biashara ya bidhaa, huduma na uhamisho mali nchi za nje inatarajiwa kufikia asilimia 4.3 ya pato la Taifa mwaka 2018/19, kutoka asilimia 3.5 ya mwaka 2017/18. Hali hii itatokana na matarajio ya

[3] Kizio cha mwaka 2007

kuongezeka zaidi kwa uagizaji wa bidhaa kutoka nje ya nchi kwa ajili ya utekelezaji wa miradi mikubwa ya ujenzi wa miundombinu. Wakati huo huo, thamani ya uagizaji wa mafuta inatarajiwa kuongezeka sambamba na ongezeko la bei katika soko la dunia pamoja na mahitaji katika uchumi.

Sekta ya kibenki inatarajiwa kuendelea kuwa imara, salama na yenye mitaji na ukwasi wa kutosha. Benki Kuu ya Tanzania itaendelea kufuatilia benki za biashara zenye viwango vya juu vya mikopo chechefu na kuhakikisha benki zote zinatumia mfumo wa kuhifadhi taarifa za wakopaji wakati wa kutoa mikopo mipya ili kupunguza vihatarishi. Benki Kuu pia itafanya uchambuzi wa kina kuhusu matokeo ya utekelezaji wa Kanuni za Kimataifa za Utoaji Taarifa za Fedha, 9 (*International Financial Reporting Standard 9*, (IFRS 9)) na kuchukua hatua stahiki katika kusimamia sekta ya fedha.

Kuhusu mifumo ya malipo, Benki Kuu inaanza zoezi la kuweka mfumo wa malipo ya papo kwa papo (*Tanzania Instant Payment System,* (TIPS)) ambao utawezesha kufanya miamala kwa gharama nafuu zaidi. Katika kuhakikisha usalama na ufanisi wa mifumo ya malipo nchini, Benki Kuu itaendelea kusimamia na kutoa leseni kwa watoa huduma wa mifumo ya malipo (mabenki na yasiyo mabenki) kwa kuzingatia kanuni chini ya mfumo wa udhibiti wa usimamizi wa kisheria wa sasa.

### *Mwenendo wa Sera ya Fedha Katika Nusu ya Pili ya Mwaka 2018/19*

Katika nusu ya pili ya mwaka 2018/19, Benki Kuu itaendelea kutekeleza sera ya fedha itakayodumisha utulivu wa mfumuko wa bei na kuongeza

ukwasi katika uchumi ili kuendeleza ukuaji wa mikopo kwa sekta binafsi na shughuli mbalimbali za uchumi. Kwa kutumia nyenzo zake, Benki Kuu itaendelea kuangalia kwa ukaribu kiasi cha ukwasi kwenye mabenki (clearing balances) ili kuleta utulivu wa riba katika soko la fedha baina ya mabenki. Utulivu wa riba katika soko la fedha baina ya mabenki ni msingi katika kutekeleza mfumo mpya wa utekelezaji wa sera ya fedha unaotumia riba ya Benki Kuu (*central bank policy* rate) katika kutoa mwelekeo wa sera ya fedha.

**Hitimisho**

Katika nusu ya pili ya mwaka 2018/19, Benki Kuu itaendelea kushirikiana kwa karibu na Serikali katika kusimamia utekelezaji wa sera ya fedha inayolenga kuongeza ukwasi katika uchumi. Hii ni pamoja na kuhakikisha kwamba riba katika soko la fedha zinabakia tulivu, na ukuaji wa ujazi wa fedha unawiana na lengo la mfumuko wa bei, pamoja na matarajio ya ukuaji mpana wa uchumi. Mwelekeo huu wa sera ya fedha unatarajiwa kuendelea kuimarisha zaidi ukuaji wa mikopo kwa sekta binafsi. Benki Kuu itaendelea pia kusimamia utekelezaji wa hatua za kuimarisha udhibiti wa vihatarishi (*risk management practices*) ili kuhakikisha kuna uwazi na ufanisi katika utoaji wa huduma za fedha, na kukuza matumizi bora ya teknolojia katika utoaji wa huduma za kifedha.

Katika hatua ya kujiandaa kutumia mfumo wa utekelezaji wa sera ya fedha unaotumia riba ya Benki Kuu (*central bank policy rate*) katika kutoa mwongozo wa sera ya fedha, Benki Kuu itaendelea kushirikiana na

wadau mbalimbali ili kuhakikisha mfumo huu unafanya kazi kwa ufanisi wa hali ya juu. Utekelezaji wa mfumo huu unategemea ufanisi wa masoko ya fedha pamoja na mawasiliano kwa wadau juu ya hatua mbalimbali zinazochukuliwa na Benki Kuu ili kutekeleza sera ya fedha.

Kutokana na hatua za kisera zinazochukuliwa na serikali kwa kushirikiana na wadau katika kuboresha sheria na kanuni za usimamizi thabiti wa shughuli mbalimbali za kiuchumi, serikali kuendelea kuwekeza kwenye miundombinu, pamoja na matarajio ya kuendelea kukua kwa uchumi wa nchi na wa dunia, ni matarajio ya Benki Kuu kuwa malengo ya sera ya fedha kwa mwaka 2018/19 yatafikiwa.

Kwa maelezo zaidi wasiliana na:
Mkurugenzi wa Utafiti na Sera za Uchumi
Benki Kuu ya Tanzania, 2 Mtaa wa Mirambo, 11884 Dar es Salaam
Simu: +255 22 2233328, +255 22 2233350, Nukushi: +255 22 2234060
Tovuti: http://www.bot.go.tz

Kimepigwa Chapa na Identity Promotion Ltd